# JARIDA MAALUM

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

www.mwt.go.tz Toleo la Septemba, 2022 Tanzania





**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Akiwapungia Wananchi Waliofika Kushuhudia Ufunguzi Rasmi wa Barabara ya Nyahua – Chaya (Km 85.4) Katika Kijiji cha Tura, Mkoani Tabora. Wengine Katika Picha ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa.**

*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, (aliyevaa koti la blue) akikagua moja ya gari linalotumia umeme asilia lililotengeneza na Chuo cha Teknolojia cha Dar es salaam (DIT), mara baada ya kufungua maadhimisho ya 19 ya siku ya wahandisi nchini, jijini Dodoma.*



# Prof. Mbarawa Awataka Wahandisi Kuibua na Kuchangamkia Fursa za Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu



*Wahandisi ndio nguzo muwe na weledi na umakini katika kusimamia miradi ili iwe bora yenye gharama nafuu na inayokamilika kwa muda uliopangwa*

**Prof. Makame Mbarawa**
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*

Na **Shukuru Senkondo** - WUU

Serikali imeahidi kuendeleza, kuibua, kutambua, kukuza na kuendeleza ubunifu unaofanywa na wahandisi wazawa kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amesema hayo leo wakati akifungua maadhimisho ya 19 ya siku ya wahandisi nchini ambapo pamoja na mambo mengine amesisitiza umuhimu wa kuzingatia sheria ya kuwawezesha wazawa katika ujenzi wa miradi ili kunufaika kiutalaamu, kiuzoefu na kiuchumi.

Prof. Mbarawa ameaigiza Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), kuchukua hatua stahiki za kisheria na za haraka kwa makampuni ya kihandisi, Taasisi na wahandisi wasio waadilifu.

Amesema serikali itaendelea kutekeleza miradi mingi ya kimkakati katika kujenga miundombinu na uchumi wa nchi hivyo ni jukumu la wahandisi kuitumia fursa hii muhimu kujenga Taifa lao.

Ameitaja baadhi ya miradi ambayo ujenzi wake unaendelea kuwa ni ujenzi wa reli ya SGR, Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, Bandari za Dar es salaam,Tanga na Mtwara, miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara, viwanja vya ndege, maji na umeme.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, amewapongeza na kuwashukuru wahandisi kwa kujenga miundombinu mingi na ya kisasa jijini Dodoma ikiwemo reli, barabara, maji na majengo pia amewataka kuzidi kujenga uaminifu ili waweze kuaminika na kupewa kazi zaidi.

Aidha, amewakaribisha kuangalia fursa za uwekezaji katika mkoa wa Dodoma ili kuuwezesha kuwa na hadhi ya makao makuu ya nchi.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) Mhandisi Balozi Aisha Amour, amesema maadhimio yote yanayotolewa kwenye maadhimisho hayo yatafanyiwa kazi kwa wakati ili kuendeleza na kuleta tija katika sekta zinazohusu wahandisi nchini.

"Tumejipanga kuhakikisha kazi nzuri zinazofanywa na wahandisi zinaendelezwa na kuhakikiwa ili ziwe kwenye ubora unaokubalika wakati wote", amesema Balozi Aisha.

Kwa upande wake Msajili wa ERB, Mhandisi Bernard Kavishe, ameeleza kuwa mpaka sasa Bodi imesajili wahandisi 33,773 ambapo kati ya hao wahandisi wanawake ni 4,012 sawa na asilimia 12.98 na kusisitiza Bodi itaendelea kuwaendeleza wahandisi wanawake.

Maadhimisho ya 19 ya Siku ya Wahandisi yanaongozwa na kauli mbiu

***"Ubunifu na Uendelezaji wa Ujuzi katika Kuimarisha Maendeleo Endelevu ya Uchumi wa Taifa: Mtazamo wa Kihandisi".***



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Balozi Aisha Amour, akisisitiza jambo kwa wahandisi (hawapo pichani), wakati wa maadhimisho ya 19 ya Siku ya Wahandisi, yaliyofanyika jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizungumza katika maadhimisho ya 19 ya Siku ya Wahandisi, yaliyofanyika leo jijini Dodoma*



*Msajili wa Bodi ya Wahandisi, Mhandisi Bernard Kavishe, akizungumza katika maadhimisho ya 19 ya Siku ya Wahandisi, yaliyofanyika leo jijini Dodoma.*




# Tanzania Yaadhimisha Siku ya Bahari Duniani

Na **Biseko Ibrahim -** WUU

Imeelezwa kuwa usafiri wa baharini umekuwa na umuhimu mkubwa katika usafirishaji wa mizigo duniani kwani takribani asilimia 80 ya biashara kimataifa hutegemea usafiri huo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya siku ya bahari duniani Wilayani Kilwa Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete, amesema kwa kutambua umuhimu huo Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa meli nane zikiwemo nne kwa Tanzania Bara na nne Zanzibar.

“Napenda kuwahakikishia kuwa Viongozi wetu wa Kitaifa wanatambua umuhimu mkubwa wa usafiri huu na uwekezaji huo ukikamilika utakuwa na manufaa kwa kuongeza pato la taifa kwa ujumla lakini pia kupunguza zaidi gharama za bidhaa zinazosafirishwa’, amesema Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete amesema pamoja na ujenzi wa meli hizo Serikali kwa Tanzania Bara inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uboreshaji wa miundombinu ya bandari za bahari ya Hindi na kwenye maziwa lengo likiwa kurahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria.

Naibu Waziri Mwakibete amelitaka Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), kuhakikisha linafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye vya usafiri majini ili kuhakikisha vinakidhi matakwa ya uendeshaji kulingana na sheria za kimataifa za usafiri huo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kilwa Bi. Zainab Kawawa, ameipongeza Serikali kwa kuendeleza miundombinu na kusema kukamilika kwake kutarahisisha usafirishaji wa bidhaa zinazozalishwa mkoani humo na itakuza utalii.

Mkuu huyo wa Wilaya ameishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuendeleza bandari ya uvuvi ya Kilwa ambayo kukumilika kwa mradi huo kutasafirisha tani elfu 60 kwa mwaka.

Naye Muwakilishi wa Katibu Mkuu wa Uchukuzi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira, Stella Katondo, amemhakikisha Naibu Waziri Mwakibete kuwa Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu shughuli za usafiri wa majini kwa kuzingatia miongozo ya Kimataifa.

Maadhimisho ya siku ya bahari Duniani yanafanyika kwa siku nne Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi ambapo kwa mwaka huu yamebeba kauli mbiu isemayo “Teknolojia mpya kwa uchukuzi baharini wa kulinda mazingira.




*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akimsikiliza Kapteni kutoka Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) Ghadaf Chambo kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na Wakala huo, wakati Naibu Waziri huyo alipotembelea banda la Shirika hilo katika maadhimisho ya Siku ya Bahari Duniani.*




*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akisalimiana na Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu ya Uchukuzi, Mhandisi Zadock Murusuri, mara baada ya kuwasili katika maadhimisho ya Siku ya Bahari Duniani yaliyoadhimishwa Kitaifa Wilayani Kilwa Mkoani Lindi.*

# Maadhimisho ya 19 ya Bodi a Usajili wa Wahandisi (ERB)



**Eng. Benard Kavishe**
*Msajili wa Bodi ya Wahandisi*

Na **Segolena Francis** - WUU

Akizungumza jijini Dodoma leo Msajili wa Bodi ya Wahandisi (ERB), Eng. Benard Kavishe, amesema maandalizi kwa ajili ya maadhimisho hayo yamekamilika ambapo takriban wahandisi 3500 kutoka ndani na nje ya nchi wanatarajiwa kushiriki.

Eng. Kavishe amesema kuwa maadhimisho hayo yatawawezesha wahandisi kuuonesha umma nini wahandisi wa Tanzania wanaweza kufanya katika kuleta maendeleo ya nchi na kukuza uchumi, kuwawezesha wahandisi kuonesho ubunifu wa teknolojia mpya zinazotumiwa na wahandisi, kuwatambua na kuwapongeza wahandisi wanaofanya vizuri katika kazi zao na kuwapongeza wanafunzi toka vyuo vikuu waliofanya vizuri katika kozi za uhandisi.

Aidha Eng. Kavishe amesema takriban wahandisi 400 watakula kiapo cha utii na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taaluma na hivyo kuuwezesha umma kujenga imani kwa wahandisi na kuthamini kazi za kihandisi.

Maadhimisho ya siku ya wahandisi mwaka huu yanaongozwa na kauli mbiu isemayo "Ubunifu na Uendelezaji wa Ujuzi katika Kuimarisha Maendeleo Endelevu ya Uchumi wa Taifa: mtazamo wa kihandisi".

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya maadhimisho hayo Eng. Benedict Mukama, amesema wahandisi kutoka nchi za Kenya, Uganda na Zambia wameshawasili nchini kuungana na wahandisi wa Tanzania na wengine watashiriki kupitia mitandao ili kuwezesha maadhimisho hayo kufuatiliwa duniani kote.



# Kasekenya Aagiza TANROADS Kutengeneza Maeneo Korofi

Na **Deniza Cyprian** - WUU

Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, amewaagiza Mameneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), nchini kutoa kipaumbele katika kutengeneza maeneo korofi ya barabara na madaraja ili yaweze kupitika kipindi chote cha mwaka.

Ameyasema hayo jijini Dodoma katika kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wakala huo ambapo amewakumbusha wajibu wao katika utekelezaji wa majukumu yao ili kutoa mchango mkubwa kwa Taifa.



*Baadhi ya Mameneja wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), wakimsikiliza Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo, jijini Dodoma.*

Aidha, Eng. Kasekenye ameagiza uongozi wa TANROADS kutoa elimu kwa wasafirishaji na wadau wote wanaotumia miundombinu ya barabara nchini kutomwaga mafuta, michanga, mawe na kokoto ambavyo vinapelekea kuharibu miundombinu hiyo.

Amewataka Mameneja hao kuendelea kuwa wabunifu, waadilifu na kusimamia kazi zao kwa ubora na kwa wakati ili kuleta matokeo chanya yatakayopelekea Sekta ya Ujenzi kupiga hatua kubwa.

*"Miundimbinu ya barabara ni kichocheo katika ukuzaji wa Sekta nyingine hivyo hakikisheni mnajenga na kukarabati maeneo yote korofi ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji", amesisitiza Eng. Kasekenya.*

"Endeleeni kutumia utaalamu wenu katika ujenzi na usimamizi wa miradi ili kuwa na miundombinu bora itayokidhi mahitaji ya vizazi vya sasa na vijavyo", amefafanua Eng. Kasekenya.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi Eng. Kasekenya, Katibu Mkuu anayesimamia Sekta ya Ujenzi, Balozi Mha. Aisha Amour ameeleza kuwa lengo la kikao hicho ni kujadili na kushauri namna bora ya kutatua kero za watumiaji wa miundombinu ya barabara ikiwemo kupeana mbinu mbalimbali za kutatua kero hizo.

Amezitaja baadhi ya kero hizo kuwa na uwepo wa matuta yasiyo na viwango, mashimo kwenye barabara na uwekaji wa alama usio sahihi katika mahali husika.

"Kikao hichi kinalenga zaidi katika kazi za matengenezo ya barabara, miradi ya maendeleo inayoendelea, usalama barabarani na matukio ya ajali hivyo tumieni fursa hii kuleta mwazo chanya yatakayoikuza Sekta", amefafanua Balozi Aisha.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour, akitoa taarifa fupi katika kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Sekta hiyo kwa Mameneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), nchini jijini Dodoma.*

Kwa upande wake, Meneja wa TANROADS, mkoa wa Dar es Salaam, Eng. Haroun Senkuku, ameeleza kuwa ofisi yake inatarajia kuongeza barabara za juu (flyover) nyingine tatu (3) ili kupunguza msongamano wa magari yanayoingia na kutoka katika jiji hilo.

Naye, Meneja wa TANROADS, mkoa wa Kilimanjaro, Eng. Motta Kyando, ameeleza kuwa kazi za matengenezo ya barabara katika mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2021/22 zimekamilika kwa asilimia 95 na kwa sasa hali ya barabara katika mkoa huo ni nzuri kwani inapitika majira yote ya mwaka.

Meneja wa TANROADS, mkoa Katavi, Eng. Martin Mwakabende, ameeleza kuwa mkoa huo unahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya kilometa 1,195 ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/23 wamepanga kutekeleza miradi 39 kati ya hiyo miradi 31 tayari imepata wakandarasi.







*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya (wa tano kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Mameneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mara baada ya kufungua kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Sekta ya Ujenzi, jijini Dodoma*



# ATCL na TCAA Zapongezwa

Na **Mwandishi Wetu** - WUU

Serikali imetakiwa kuiwezesha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL), kwa kuiwekea mazingira rafiki ya kujiendesha kwa kuweka watendaji wenye mtazamo wa kibiashara.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Seleman Kakoso mara baada ya kupokea taarifa ya utendaji ya kampuni hiyo na taarifa ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), ambapo pamoja na mambo mengine amezipongeza taasisi hizo kwa kazi nzuri wanazozifanya katika utoaji wa huduma bora kwa wadau na udhibiti wa usafiri wa anga nchini.

"Serikali wekezeni zaidi katika Kampuni ya ATCL ili iweze kufanya vizuri zaidi kibiashara na isaidieni kumaliza madeni yaliyokuwepo kipindi cha nyuma", amesisitiza Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Kakoso. Aidha, Kamati hiyo ya Miundombinu imezungumzia umuhimu wa Serikali kuendelea kusimamia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), katika uboreshaji wa viwanja vya ndege vinavyoendelea kujengwa ikiwemo vya Iringa na Musoma na kusisitiza kasi katika ujenzi wake.

"Simamieni kwa karibu ujenzi wa viwanja vya ndege hapa nchini ili kuiwezesha ATCL kufanya vizuri kwa kuwa ufanisi wa kampuni hiyo unahitaji ubora wa viwanja vya ndege nchini", amefafanua Mhe. Kakoso.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete, ameieleza Kamati hiyo kuwa ujenzi na uboreshaji wa baadhi ya viwanja vya ndege hapa nchini vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake na Serikali tayari imepata fedha za uboreshaji wa viwanja vya Ndege vya Tanga na Lindi.

Awali akitoa taarifa ya Utendaji wa Kampuni ya ATCL, Afisa Mtendaji Mkuu wa ATCL Eng. Ladislaus Matindi ameieleza Kamati hiyo kuwa Kampuni imefanikiwa kufanya ushirikiano wa kibiashara na makampuni saba (7), ya ndege ambayo ni Qatar Airways, Air India, Emirates, KLM, Omani Air, Rwanda Air na Ethiopian Airlines ambapo mashirikiano hayo yamelenga

kuhakikisha muungano wa safari kwa abiria wa ATCL na mashirika hayo katika maeneo ambayo ATCL itakuwa haifanyi safari zake.

Ameongeza kuwa Kampuni hiyo imeongeza vituo na kufanya mtandao wa safari wa ATCL kufikia vituo 26 ambapo vituo 15 vya ndani na tisa (9) ni vya nje.

Amevitaja vituo hivyo kuwa ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Mpanda, Mwanza, Mtwara, Songea, Tabora na Zanzibar wakati vya nje ni Bujumbura, Entebbe, Hahaya, Harare, Lusaka, Ndola, Nairobi, Johannesburg na Lubumbashi na vituo viwili (2) ni vya nje ya Afrika nchi ambavyo ni Mumbai - India na Guangzhuo - China.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Bw. Hamza Johari, ameileza Kamati hiyo kuwa Mamlaka imefanikiwa kusaini upya mkataba ya usafiri wa anga kati yake na nchi nyingine ili kufungua soko la usafiri wa anga kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri wa anga, kuvutia mashirika mengine kutoa huduma nchini na kuimarisha ushindani katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

Hamza ameongeza kuwa Mamlaka imefanikiwa kutoa leseni mpya 1,223 na kuhuisha leseni 270 katika fani mbalimbali katika Sekta ya usafiri wa anga.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imepokea, kujadili na kushauri taarifa ya utendaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Selemani Kakoso*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, akizungumza jambo na Naibu Katibu Mkuu wa Uchukuzi, Dkt Ally Possi, wakati wa kikao cha kuwasilisha taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utendaji kazi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga wa Tanzania (TCAA), na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), jijini Dodoma.*

# Katibu Mkuu Uchukuzi Awataka ATCL Kushughulikia Changamoto



Na **Christopher Philemon** - WUU

Katibu Mkuu wa Uchukuzi Gabriel Migire amemtaka Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kuhakikisha anafanya tafiti za mara kwa mara ili kupata suluhu ya changamoto mbalimbali zinazolikabili shirika hilo.

Akizugumza mjini Morogoro wakati wa kufunga Baraza la Wafanyakazi wa ATCL, Katibu Mkuu huyo amesema changamoto hizo zinazohusisha uchelewaji wa ratiba za kuruka na kutua ndege, huduma kwa wateja na uadilifu zinahitaji ufumbuzi wa haraka kwani zimekuwa zikififisha ubora wa utendaji wa shirika hilo.

"Serikali ilifanya maamuzi ya kulifufua shirika hili kutoka kutokuwa na ndege mpaka kuendesha ndege zaidi ya 10 hivi sasa, lakini kila wakati tumekuwa tukisikia changamoto nyingi kutoka kwa wateja wa ndani na nje ya nchi hivyo katika Baraza hili mpange mikakati ya kuhakikisha changamoto hizi zinapata ufumbuzi mapema", amesisitiza Katibu Mkuu Migire.

Katibu Mkuu Migire amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan itaendelea mikakati yake ya kulifufua shirika hilo kwa kuhakikisha ndege tano zilizobaki zinakuja ili kulifanya shirika hilo kuchangia katika sekta mbalimbali ikiwemo Kilimo na Utalii.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa ATCL Mhandisi Ladislaus Matindi, amesema kwa sasa Shirika limeendelea kukua kwani mpaka sasa kwa mtandao wa ndani shirika linatoa huduma kwa zaidi ya viwanja 12, kanda vituo zaidi ya 6 na nje vituo viwili.

Mhandisi Matindi ameongeza kuwa kwa sasa shirika limekuja na mpango wa miaka mitano ulioanza Julai 2022 hadi June 2026 ambapo msisitizo umewekwa kwenye mpango wa mwaka mmoja wa 2022/23 ambao unajielekeza kuongeza vituo vya ndani kufikia zaidi ya 19 kutoka vituo

14 vya sasa.

Naye Katibu wa Baraza la Wafanyakazi wa ATCL Bw. Margret Leslie, amesema kwa upande wa wafanyakazi wanaendelea kuchapa kazi kwa weledi na ubunifu ili kuhakikisha Shirika linakidhi vigezo vya utoaji huduma vilivyowekwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO).

Baraza la wafanyakazi la ATCL limekutana kwa siku mbili mjini Morogoro ambapo pamoja na mambo mengine limeweka mipango mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa huduma nchini na nje ya nchi.









# Kamati ya Miundombinu Yashauri TBA Ujenzi wa Nyumba za Kisasa

Na **Siti Said** - WUU

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeutaka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuhakikisha inajenga nyumba za kisasa ambazo zinaendana na uhalisia ili kukidhi mahitaji ya washitiri wake.

Hayo yamesemwa jijini Dodoma na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Suleiman Kakoso, mara baada ya Kamati hiyo kupokea taarifa ya utendaji kazi wa Wakala huo pamoja na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA).

Mheshimiwa Kakoso, amesema kuwa sambamba na hilo Wakala huo umetakiwa kuhakikisha unaongeza ubunifu katika utekelezaji wa miradi yake ili kuweza kukidhi soko la ushindani nchini na nje ya nchi.

"Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa miradi yenu, ila hakikisheni mnaweka mikakati inayotekelezeka kwani uwekezaji kwenye ujenzi wa nyumba unakuwa na kubadilika kila siku hivyo mnatakiwa mwende sambamba na mabadiliko hayo ili kuweza kupata wateja ndani na nje ya nchi", amesema Kakoso.

Aidha, Kakoso ameutaka Wakala huo pia kuhakikisha wanaendeleza na kubuni miradi mbalimbali katika maeneo ambayo wanamiliki ili kulinda maeneo yao pamoja na kusambaza huduma maeneo mbalimbali nchini.

Kuhusu utendaji wa kazi wa TEMESA, Kamati imeishauri Wizara kuusimamia kwa karibu Wakala huo ili kuweza kuleta tija na kupunguza na changamoto ambazo zinaukabili.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Selemani Kakoso, akisisitiza jambo wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya utendaji kazi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), jijini Dodoma.*

Kwa upande wake, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, amesisitiza TBA kuendelea kuwa wabunifu kwa kuhakikisha unaendelea kujenga na kukarabati nyumba na majengo ya Serikali ili kuongeza ubora wa makazi kwa viongozi na watumishi wa umma.

Waziri Mbarawa ametaja miradi ya kitaifa mikubwa ambayo imetekelezwa na TBA kuwa ni ujenzi wa nyumba za makazi za Magomeni Kota, jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya SekouToure Mwanza, jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Ujenzi wa makazi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne na Usimamizi wa mradi wa ujenzi wa Ikulu Chamwino Dodoma.

Kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) Waziri Mbarawa ameushauri Wakala huo kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika uendelezaji wa karakana zao kama walivyofanya kwenye vivuko kwa kuruhusu Kampuni ya Azam Marine

kutoa huduma za usafirishaji kati ya Magogoni na Kigamboni jijini Dar es salaam na hivyo kupunguza malalamiko ya wateja.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imepokea, kujadili na kushauri taarifa ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuhusu masuala mbalimbali ya kiutendaji ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA).



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akifafanua jambo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.*



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akiwasilisha taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya utendaji kazi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), jijini Dodoma.*



*Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakifuatilia taarifa ya utendaji kazi iliyowasilishwa kwao na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), katika ukumbi wa Utawala wa Bunge, jijini Dodoma.*

# MSCL Yatakiwa Kutumia Meli kwa Tija




Na **Biseko Ibrahim -** WUU

Serikali imeitaka Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuhakikisha inazitumia kwa tija meli tatu ilizokabidhiwa ili ziweze kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa wakazi wanaozunguka Ziwa Nyasa na Nchi Jirani.

Meli hizo ambazo zimegharimu zaidi ya shilingi bilioni 10 ni MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 200 na mzigo wa tani 200, Mv. Ruvuma yenye uwezo wa kubeba mzigo wa tani 1000 na MV.Njombe yenye uwezo wa kubeba mzigo wa tani 1000.

Akizungumza Wilayani Kyela, Mkoani Mbeya wakati wa makabidhiano hayo Mwakilishi wa Katibu Mkuu (Uchukuzi) ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Mazingira -Uchukuzi Bi. Stella Katondo amesema kukabidhiwa kwa meli hizo katika kampuni hiyo inamaanisha kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ambaye ndio mmiliki kubaki na kazi ya usimamizi wa bandari tu.

“Jukumu la TPA ni kusimamia bandari nchini si kuendesha meli ndio maana baada ya kukamilika kwa ujenzi wa meli hizi, Serikali ikaamua kuwakabidhi MSCL ambao ndio wenye dhamana ya kuendesha meli hizi, ni matumani yangu kuwa meli hizi zitatumika ipasavyo na tutaona thamani ya uwezekezaji huu”, amesisitiza Mkurugenzi Katondo.

Mkurugenzi Katondo amezitaka TPA na MSCL kuchukua jitihada za haraka za kutafuta na kushawishi wafanyabiashara wa makaa ya mawe na simenti ili kutumia meli hizo ili kusafirisha mzigo mkubwa zaidi, kwa gharama zinazohimilika na hatimaye kuwafikia walaji kwa wakati.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Kyela Mhe. Ally Mlaghila amesema kukabidhiwa kwa meli hizo kwa MSCL kutaongeza tija kwa uendeshaji kwani kampuni hiyo ina uzoefu mkubwa wa uendeshaji wa meli katika Ziwa Nyasa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Plasduce Mbossa amesema tayari TPA imeshaanza mazungumzo na wafanyabiashara wa ndani na nchi zinazotumia ziwa Nyasa ili kuhakikisha mzigo unapatikana na zinatumika.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu MSCL Kapteni Samson Ng’wita, ameishukuru Serikali kwa kufanya maamuzi hayo na kusema kwamba MSCL iko tayari kuanza kuendesha meli hizo na kuahidi huduma bora na za viwango kwa abiria na wafanyabiashara.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Plasduce Mbossa (kulia), akikabidhiana na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu MSCL Kapteni Samson Ng'wita, mkataba wa makabidhiano ya MV. Ruvuma, MV Mbeya II na MV Njombe, katika Bandari ya Kiwira, Wilayani Kyela, Mkoani Mbeya.*




*Muonekano wa meli ya mizigo ya MV Njombe. Meli hiyo ina uwezo wa kubeba mzigo wa tani 1000 kwa wakati mmoja na inafanya safari zake katika Bandari za Ziwa Nyasa na Nchi Jirani zinazonguka ziwa hilo.*

Makabidhiano hayo ya meli hizo tatu yamefanyika katika bandari ya Kiwira na kushuhudiwa na Uongozi wa Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Kyela, Mbunge wa Kyela, Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango-Hazina, Katibu wa Chama Cha Mpainduzi -Kyela.

# Katibu Mkuu Ujenzi Afunga Kikao Kazi na Mameneja wa TANROADS Jijini Dodoma





*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Aisha Amour, akisaini na kumkabidhi mkataba wa utendaji na Mtendaji Mkuu wa Barabara Nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, mara baada ya kufunga kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Jijini Dodoma.*



*Mtendaji Mkuu wa Barabara Nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila (kushoto), akimkabidhi mkataba wa utendaji kazi Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Arusha, Mhandisi Reginad Massawe, mara baada ya kufunga kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour, akizungumza wakati akifunga kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo kati ya sekta hiyo na Mameneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), nchini jijini Dodoma.*

# Katibu Mkuu Uchukuzi Asaini Mikataba ya Utendaji na Wakuu wa TMA, TASAC na NIT



*Katibu Mkuu-Uchukuzi, Gabriel Migire (kushoto waliokaa) akisaini Mkataba wa Utendaji na Mkuu wa Chuo cha Taifa Cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa, katika Ofisi za Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu-Uchukuzi, Gabriel Migire (kushoto waliokaa) akisaini Mkataba wa Utendaji na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Dkt Agness Kijazi katika Ofisi za Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu-Uchukuzi, Gabriel Migire (kushoto waliokaa) akisaini Mkataba wa Utendaji na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Kaimu Mkeyenge katika Ofisi za Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, jijini Dodoma.*



# Prof. Mbarawa: TANROADS Fanyeni Tafiti Kupunguza Ajali za Barabarani

Na **Deniza Cyprian** - WUU

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, ameitaka Wakala wa Barabara (TANROADS), nchini kuhakikisha wanafanya utafiti katika eneo la Shamwengo karibu na kituo cha mafuta Inyala, mkoani Mbeya ili kupunguza ajali zinazotokea mara kwa mara eneo hilo.

Waziri Mbarawa amaeyasema hayo jijini Dodoma, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombionu baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka kwa Wakala huo na Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) zilizowasilishwa leo, Bungeni jijini humo.

"Ni kweli hapa changamoto zimekuwa kubwa katika eneo hilo na Serikali haifumbii macho ajali zinazoendelea kutokkea kwenye eneo hilo, sasa TANROADS fanyeni tafiti ili kupata majibu ya haraka ili kutatua changamoto hii", amesema Prof. Mbarawa.

Amesisitiza Wakala huo kuhakikisha wanaweka alama za barabara kwenye miundombinu hiyo ili kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara pindi inapoharibika.

Aidha, Profesa Mbarawa amesema kuwa Serikali kupitia Wakala huo bado inaendelea na ukarabati na matengenezo ya barabara katika maeneo mbalimbali nchini hususan yenye miinuko na kona kali lengo ni kusaidia kupunguza ajali zinazoweza kujitokeza katika maeneo hayo.

Kuhusu utekelezaji wa miundombinu hiyo nchini jumla ya miradi 17, ilipata kibali cha ujenzi kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2020/21 ambapo hadi kufikia 22 Agosti, 2022 miradi 13 yenye mikataba ya thamani ya takribani Shilingi Bilioni 641 ilikuwa imesainiwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Suleiman Kakoso ameitaka Wizara kuhakikisha wanatoa kipaumbele cha ujenzi wa barabara katika maeneo ya kimkakati ili kuhakikisha miundombinu inasambaa nchini kote na wananchi wote kupata maendeleo kwa usawa.

"Hakikisheni mnazingatia Sera ya Ujenzi wa miundombinu kuweka kipaumbele katika kuunganisha mikoa kwa mikoa, wilaya kwa

wilaya, nchi kwa nchi na maeneo yenye uzalishaji", amefafanua Mhe. Kakoso.

Ameitaka Wizara hiyo kuhakikisha inasimamia Sheria ya Barabara katika kulinda miundombinu hiyo ambayo kwa namna moja ama nyingine inaathiriwa na shughuli za kibinadamu na hivyo kupelekea kuharibika mapema kwa miundombinu hiyo.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imepokea, kujadili na kushauri taarifa ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuhusu masuala mbalimbali ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT).



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akifafanua jambo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati wa kamati hiyo ilipopokea taarifa ya utendaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT), pamoja na utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja nchini, jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Selemani Kakoso (kulia), akizungumza na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya utendaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT), pamoja na utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja nchini, jijini Dodoma*

## Naibu Waziri Atupele Atembelea Bandari na Kiwanja cha Ndege Kilwa



*Muonekano wa Barabara ya kuruka na kutua ndege yenye urefu wa Kilomita 1850 katika Kiwanja cha Ndege cha Kilwa.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (wa kwanza kulia) akimsikiliza Ofisa Ulinzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Theophil Kaiza kuhusu shughuli za utendaji wa bandari ya Kilwa Masoko wakati Naibu Waziri alipotembelea bandari hiyo Wilayani Kilwa Mkoani Lindi.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akitoa maelekezo kwa Ofisa Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko Shaban Said (mwenye shati la mistari) kuhusu utendaji wa kiwanja hicho wakati Naibu Waziri alipotembelea bandari hiyo Wilayani Kilwa Mkoani Lindi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kilwa Zainab Kawawa.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akimsikiliza Ofisa Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko Shaban Said kuhusu utendaji wa kiwanja hicho wakati Naibu Waziri alipotembelea bandari hiyo Wilayani Kilwa Mkoani Lindi.*

# Mhandisi Kasekenya Ahimiza Teknolojia Mpya Kupenya Vijijini



Na **Shukuru Senkondo** - WUU

Naibu Waziri wa Ujenzi Mhandisi, Godfrey Kasekenya amezungumzia umuhimu wa wahandisi nchini kubuni teknolojia rahisi zinazoweza kutatua changamoto za maisha ya Wananchi vijijini na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo nchini.

Akifunga mkutano wa 19 wa Wahandisi jijini Dodoma Mhandisi, Kasekenya amesema maendeleo ya kimkakati nchini yatafikiwa endapo ubunifu na teknolojia zitawanufaisha wananchi wengi hususan waishio vijijini.

"Hakikisheni teknolojia hizi nzuri mnazoonesha mwaka hadi mwaka zinaweza kutumiwa kikamilifu na wananchi waishio vijijini na wenye kipato cha chini ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na kuleta maendeleo kwa taifa zima" amesisitiza Mhandisi Kasekenya.

Naibu Waziri huyo ameitaka Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), kuwasilisha mapendekezo yote yaliyotolewa katika mkutano huo wa siku mbili Wizarani ili yaweze kupatiwa ufumbuzi wa haraka ili kuleta tija kwa kada ya wahandisi nchini.

Amezungumzia umuhimu wa Wahandisi kuungana ili kunufaika kwa mitaji, uzoefu na hivyo kuwa na nguvu ya pamoja itakayowawezesha kukua na kukuza teknolojia ndani na nje ya nchi.

*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, akikabidhi zawadi mbalimbali kwa washiriki mara baada ya kufunga maadhimisho ya 19 ya siku ya wahandisi nchini yaliyofanyika jijini Dodoma.*





*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya , akikagua moja kati ya banda la maonesho ya teknolojia mara baada ya kufunga maadhimisho ya 19 ya siku ya wahandisi nchini yaliyofanyika jijini Dodoma.*

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Sekta ya Ujenzi Eng, Balozi Aisha Amour amewataka washiriki wa mkutano huo kutumia maarifa waliyoyapata katika utekelezaji wa majukumu na kutoa elimu waliyoipata kwa wahandisi wengine ili kujenga uelewa wa pamoja katika jamii ya wahandisi nchini.

Msajili wa Bodi ya Wahandisi (ERB) Eng. Bernard Kavishe amesema zaidi ya makampuni 70 yameshiriki kuonesha bidhaa za kiteknolojia katika maonesho hayo na wahitimu 36 waliofanya vizuri katika vyuo mbalimbali vya kihandisi nchini wametunukiwa zawadi mbalimbali ikiwa ni chachu ya kuwahamasisha wanafunzi nchini kupenda fani ya uhandisi.

Mkutano huo wa siku mbili uliomalizika leo umeongozwa na kauli mbiu isemayo "ubunifu na Uendelezaji wa Ujuzi katika kuimarisha Maendeleo Endelevu ya Uchumi wa Taifa: mtazamo wa kihandisi"





*Wajumbe wa Kamati ya Mapendekezo ya Ujenzi wa Mabwawa katika maeneo yanayopata changamoto ya mafuriko na kuathiri miundombinu ya reli kipande cha Dabalo, Chalinze Buigili na Hombolo wakikagua eneo linalopendekezwa kujengwa Mabwawa hayo, Mkoani Dodoma.* **Picha na WUU.**


MT SANGARA

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**
**Mji wa Serikali Mtumba**
**S.L.P 2888 Ujenzi / S.L.P 638 Uchukuzi**

# DODOMA

**Simu: +255 26 23244455 / +255 26 2322703, 2322702**
**Nukushi: +255 26 2323233 / +255 26 2322704**
**Barua pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwt.go.tz**

wizarayaujenzinauchukuzi
wizaraUJnaUC
www.mwt.go.tz